**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

Simu Na: +255 737959943
**"AFYA"**

E-mail: manyararrh@afya.go.tz
Website: www.manyararrh.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:-

Hospitali ya Mkoa Manyara,
S.L.P. 577
**BABATI.**

**Kumb. Na. MRRH/I20/14/13** **08 Aprili, 2022**

**Katibu Mkuu,**
Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto,
Mji wa Serikali Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L.P. 743,
**40478 DODOMA.**

Yah: **MAOMBI YA FEDHA SHILINGI 87,800,000 KWA AJILI YA MANUNUZI YA "BLOOD GAS ANALYZER", "BED AND MATRESS", "CABINETS" NA "CARDIAC TABLES"**

Husika na mada tajwa hapo juu,

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Manyara imefanya taratibu za manunuzi kwa ajili ya vifaa na mashine tajwa hapo juu kama ilivyobainishwa kwenye mpango wa fedha za IMF. Naleta kwako maombi ya fedha kwa ajili ya manunuzi ya vifaa na mashine hizo Maombi ya fedha hizo ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:-

| NA | AINA YA MASHINE/KIFAA | IDADI | KIASI/MOJA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | BLOOD GAS AND ELECTROLYTES ANALYSER | 1 | 19,500,000 | 19,500,000 |
| 2 | BLOOD GAS ANALYSER | 1 | 19,000,000 | 19,000,000 |
| 3 | BED AND MATRESS | 19 | 1,800,000 | 34,200,000 |
| 4 | CARDIAC TABLES | 19 | 300,000 | 5,700,000 |
| 5 | BED SIDE CABINETS | 22 | 250,000 | 5,500,000 |
| 6 | USAFIRISHAJI, KUFUNGA NA MAFUNZO | | 3,900,000 | 3,900,000 |
| | JUMLA | | | **87,800,000** |

Pamoja na barua hii naambatisha muhtasari wa kamati ya Tiba na Dawa, mkakati wa kukabiliana na upandaji wa bei, mkakati wa ufuatiliaji wa miradi, nukuu za bei na mikataba ya manunuzi ya vifaa/mashine.

Nawasilisha kwa hatua zaidi.

Dkt. Katherine T. Magali
**MGANGA MFAWIDHI**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA**

## MKAKATI WA KUKABILIANA NA UPANDAJI WA GHARAMA ZA VIFAA VYA UTEKELEZAJI WA MRADI

Hospitali imejipanga kufanya yafuatayo:-

1. Kuingia mkataba na mzabuni ukiwa na kipengele kitakachoonesha kuwa bei za mkataba wa mwanzo hazitabadilika endapo bei za soko zitapanda au kupungua
2. Kuhakikisha mzabuni anajaza bei za soko zilizopo muda ambao anajaza bei

## MKAKATI WA USIMAMIZI NA UFATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MRADI

Lengo la usimamizi na ufuatiliaji wa mradi ni kupima utendaji wa watekelezaji wa miradi, hatua za utekelezaji na changamoto zinazoukabili mradi ili kuzitatua kwa wakati na kuepuka kusimama kwa mradi.

**MIKAKATI**

a) kuunda timu ya usimamizi na ufuatiliaji ikiongozwa na Katibu Tawala Mkoa na Mganga Mfawidhi. Ufuatiliaji utakuwa shirikishi ukiwa na timu ya mkoa na hospitali ambayo itatembelea kila siku, wiki, mwezi, miezi mitatu (kila robo mwaka) hadi mwisho wa utekelezaji wa utekelezaji wa mradi.

b) Timu ya ufuatiliaji ikiongozwa na Mwenyekiti wao itakuwa na mfumo wa mrejesho wa utekelezaji wa mradi kwa kuandaa taarifa za utekelezaji, kupiga simu na kupata picha za hatua mbalimbali za utekelezaji.

c) Kufanya vikao vya tathmini kila wiki, mwezi, miezi mitatu (quarterly) ili kupima kiwango cha utekelezaji wa mradi kulingana na malengo ya mradi, fedha zilizotolewa, muda uliokusudiwa na matokeo yaliyokusudiwa.

d) Kutoa mapendekezo katika ngazi ya Mkoa na Wizara juu ya utatuzi wa changamoto zinazoukabili mradi ili kuwezesha mradi kukamilika kwa wakati.

e) Timu za uratibu, uendeshaji na usimamizi wa mradi kuandaa taarifa ya mradi kila mwezi na kuiwasilisha kwa Katibu Tawala na Katibu Mkuu Wizara ya Afya. Taarifa hizo zitaonesha kazi zilizopangwa, hatua za utekelezaji, kazi zilizokamilika, kazi zinazoendelea, changamoto na mikakati/mapendekezo ya kutauta changamoto hizo.

# KIKAO CHA HOSPITAL FORMULARY TAREHE 06/04/2022

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 7:30 mchana.

Kikao kilianza kwa mrejesho kutoka kila idara ambapo idara nyingi zilikua hazijakamilisha kuandika dawa na matumizi yake kama inavyotumika katika idara. Mwenyekiti aliongeza muda ili kila idara iwasilishe kazi hiyo. Siku ya Jumatatu ya tarehe 11/04/2022 tutakutana tena kwa ajili ya kuwasilisha na kuzipitia kwa pamoja.

Mjumbe mmoja aliuliza juu ya mfumo rasmi unaotumika katika kuainisha dawa na mwenyekiti alieleza kua dawa zinatakiwa kuwekwa katika makundi kutokana na matumizi.

Mjumbe mwingine aliuliza kama POP, splint navifaa vya Orthopedic vinafaa kuingizwa kwenye hospital formulary.

Jibu: Hizo ni medical supplies. Medical supplies zimekua limited kuingia kwenye hospital formulary hivyo wajumbe walipendekeza kushirikishwa kwa kamati ya Logistics, Supplies and Capacity building katika kuhakikisha upatikanaji wa vifaa hivi.

Mnamo saa 8:38 mchana kikao kilikaimishwa jukumu la kujadili juu ya manunuzi ya wheelchair na manunuzi ya vifaa tiba ikiwepo cardiac table, vitanda na bedside cabinet.

**Manunuzi ya Wheelchair**

Suala ni kujadili zinunuliwe wapi kati ya KCMC na kiwandani. Wajumbe wengi walipendekeza zinunuliwe kutoka KCMC.

**Manunuzi ya vifaa tiba vya thamani ya Milioni 87,800,000.**

Mjadala mkuu ulikua juu ya aina ya Blood gas analyzer ya kununua, na ni ngapi zinunuliwe.

Makubaliano: kununua 2 kutoka kampuni mbili tofauti.

Cardiac tables 19, bedside cabinet 22 na vitanda 19.

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 9:30 alasiri.

Mwenyekiti wa kamati ya drug formulary

.............................

Dr Yesige Mutajwaa

Katibu wa kikao

CMWanjara
.............................

Dr Caroline Wanjara

**MAHUDHURIO YA KIKAO CHA DRUG FORMULARY COMMITTEE KATIKA UKUMBI WA HOSPITALI TAREHE 06 APRILI, 2022**

| NA | JINA KAMILI | CHEO | SAHIHI |
|---|---|---|---|
| 1. | Dr Yonge Mulugwa | M/kiti | [illegible] |
| 2 | Sofia M. Mmbali | Mjumbe | [illegible] |
| 3 | Athanas Andrea Budodi | Mjumbe | [illegible] |
| 4 | Edward M. Magoma | Mjumbe | [illegible] |
| 5. | BABU M. MENGORIKI | Mjumbe | [illegible] |
| 6 | Caroline Wanjara | Caroline | C.N.Wanjara |
| 7. | LUDOVICK LEGAMA | Mjumbe | [illegible] |
| 8 | Bernadetha Kahwa | Mjumbe | [illegible] |
| 9 | Fransiska Fabiano | Mjumbe | [illegible] |
| 10 | Denis M Jeremiah | Mjumbe | [illegible] |
| 11 | NEWTON N. SAM | 〃 | [illegible] |
| | | | |

MAHUDHURIO

| NA | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1 | DR YESIGE MUTAJWAA | M/KITI |
| 2 | DR CAROLINE WANJARA | KATIBU |
| 3 | DR SABINA M. MMBALI | MJUMBE |
| 4 | DR ATHANAS BUDODI | MJUMBE |
| 5 | DR LUDOVICK LEGAMA | MJUMBE |
| 6 | DR BABU MELEYEKI | MJUMBE |
| 7 | FRANSISKA FABIANO | MJUMBE |
| 8 | BERNADETHA KAHWA | MJUMBE |
| 9 | DR EDWARD MAGOMA | MJUMBE |
| 10 | DENNIS | MJUMBE |

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

MKATABA WA UNUNUZI WA VIFAA TIBA (BLOOD GAS ANALYZER)
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA

BAINA YA

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MANYARA

NA

MOKASI MEDICAL SYSTEMS AND ELECTRONICS SERVICES LIMITED

…………………………………………

ataba Huu Umeingiwa leo Tarehe ...08....... Mwezi ...04... 2022

ATI YA

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MANYARA** (ambaye atajulikana kama Mnunuzi kwa upande mmoja.)

NA

**MOKASI MEDICAL SYSTEMS AND ELECTRONICS SERVICES LIMITED** wa **S.L.P** ...1778... **Dar Es Salaam** (ambaye atajulikana kama Mzabuni kwa upande mwingine).

**KWA KUWA** Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara iko tayari na inania na Inahitaji Vifaa tiba Na kampuni ya **MOKASI MEDICAL SYSTEMS AND ELECTRONICS SERVICES LIMITED** itahitajika kufanya uuzaji wa Vifaa hivyo vyote kwa masharti yatakayo ainishwa kwenye mkataba huu.

**NA KWA KUWA** kampuni iko tayari na inania na uwezo wa kuuza vifaa tiba hivyo kwa kuzingatia makubaliano na masharti kama yalivyoainishwa hapa chini.

**SASA WAHUSIKA WANAKUBALIANA YAFUATAYO;**

**1.0. MAELEZO YA VIFAA HIVYO**

1.1. Mkataba huu utakuwa ni usambazaji wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara.

1.2. Vifaa tiba ambavyo mzabuni ataleta katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara ni kama ilivyo orodheshwa hapa chini;

| Na | Aina ya kifaa | Idadi | Gharama |
|---|---|---|---|
| 1 | Blood gas and electrolyte analyzer | 1 | 18,510,000.00 |
| | Test Cartrige BG 10(25PCS/PACK) BLOOD GAS & ELECTRONIC | 1 | 660,000 |
| | Calibrant Fluid Pack Cp 100 (100 test/pack (11/12) | 1 | 330,000 |
| | **Jumla** | | **19,500,000.00** |

**NA KWA KUWA** Mzabuni yuko tayari na ana uwezo wa kufanya kazi hiyo:

**HIVYO BASI, WAHUSIKA WANAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

**1: MAELEZO YA KAZI.**

Kazi zinazotakiwa kufanyika ni kama ifuatavyo:

a) Kusambaza vifaa tiba (blood gas analyzer) mpaka eneo husika.

b) Kuvifunga na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa vifaa tiba husika

c) Vifaa tiba vitakavyouzwa viwe vimekidhi viwango vya ubora kama ulivyoelekezwa kwenye nukuu za bei.

2: MUDA WA KUKAMILISHA KAZI/MUDA WA MKATABA.

**Mzabuni** amekubaliana na **Mnunuzi** kuleta vifaa tiba tajwa hapo juu ndani ya miezi miwili, kuanzia pale mkataba utakapo sainiwa. Ieleweke wazi kuwa **Mzabuni** akishindwa kukamilisha kazi/usambazaji wa vifaa tiba (blood gas analyzer) kwa muda waliokubaliana na **Mnunuzi**, atawajibika kumlipa Mnunuzi fidia ya ucheleweshaji (liquidated damage) ya asilimia moja (1%) ya gharama kwa siku kwa kila siku inayoongezeka baada ya kuvunja kipengele hiki cha Mkataba hadi atakapokamilisha kazi husika.

3. MALIPO KWA MZABUNI:

Mzabuni atalipwa malipo yake yote pale tu atakapomaliza kuleta vifaa vyote katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara na Hospitali kukagua na kujiridhisha kuwa vifaa vilivyoletwa vipo kwa mujibu wa mkataba wake ndipo Mzabuni atalipwa malipo yake ambayo ni kiasi cha **Tsh 19,500,000/=(Milioni kumi na tisa na laki tano tu )**

4. MAJUKUMU YA WAHUSIKA:

4.1 Majukumu ya Mzabuni

**Mzabuni atatakiwa:**

(a) Kutoa Huduma inayohitajika na Mnunuzi kwa wakati na muda waliokubaliana.

(b) Kutoa Huduma kwa viwango vilivyooneshwa na ubora unaotakiwa na Mnunuzi

(c) Kuzingatia suala la muda katika kutekeleza huduma hiyo.

(d) Kuzingatia uangalifu, uadilifu na uaminifu wakati wa kutekeleza Mkataba huu. Itakapobainika kuna udanganyifu katika kutekeleza kazi hii kinyume na makubaliano yaliyomo kwenye Mkataba huu, Mzabuni atalazimika kurejesha gharama zote za Mkataba huu na kufikishwa katika vyombo vya Sheria kwa hatua za kisheria zaidi;

4.2 MAJUKUMU YA MNUNUZI.

**Mnunuzi atatakiwa:**

(a) Kumuwezesha Mzabuni kuwa na mazingira mazuri katika utekelezaji wa Mkataba huu, ikiwa ni pamoja na kukagua ubora wa huduma na kutoa ushauri au maelekezo pale inapohitajika kulingana na mahitaji ya Mnunuzi.

(b) Kumlipa Mzabuni stahiki yake kama makubaliano yalivyo. Ieleweke kuwa Mnunuzi hatalipa malipo yoyote Kwa Mzabuni kabla ya kukamilisha kuleta vifaa kulingana na Mkataba huu. Aidha, Mnunuzi hatalipa kiasi chochote cha malipo kwa Mzabuni kama Mzabuni atashindwa kukamilisha kazi kwa wakati kulingana na Mkataba badala yake Mzabuni atatakiwa kulipa fidia ya ucheleweshaji vifaa kwa Mnunuzi.

(c) Kukagua Vifaa tiba vinavyoletwa na Mzabuni na kutoa ushirikiano unaofaa wakati Mnunuzi atakapohitaji kufanya hivyo.

## 5. MATUKIO YASIYOTARAJIWA (FORCE MAJEURE)

5.1 Matukio yasiyotarajiwa ***(FORCE MAJEURE)*** yana maana ya matukio yaliyo nje ya uwezo wa wahusika na ambayo hawakuweza kuyaona wakati wa kusaini Mkataba huu, ambapo matokeo yake yatasababisha Mzabuni asiweze kutekeleza Mkataba huu. Matukio hayo ni kama vita, vita vya kikabila, moto, mafuriko, mgomo, magonjwa ya mlipuko, Mabadiliko ya Sheria na mengineyo.

5.2 Matukio haya yatakapotokea wahusika wa Mkataba huu wataahirisha utekelezaji wa Mkataba huu bila kuwajibika kwa hasara itakayotokana na tukio husika, kwa kipindi na eneo linalohusika na lililoathiriwa na tukio husika.

5.3 Wahusika wa Mkataba huu watapeana taarifa haraka iwezekenavyo kabla ya kusimamisha kazi/ huduma. Kama taarifa ya awali imetolewa kwa njia isiyo ya maandishi, ndani ya masaa 24 taarifa iliyotolewa kwa njia isiyo ya maandishi itolewe kwa maandishi. Mawasiliano yote ya maandishi yatawasilishwa kwenye ofisi ya Mnunuzi na siyo sehemu nyingine yoyote.

## 6. UWAJIBIKAJI WA WAHUSIKA.

6.1 Mzabuni atawajibika kwa hasara, uharibifu na gharama zinazotokana na uzembe wake mwenyewe, mawakala wake au wafanyakazi wake wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu.

6.2 Mnunuzi hatawajibika kwa hasara au uharibifu wowote utakaotokana na uzembe wa Mzabuni mwenyewe au Mawakala wake au wafanyakazi wake wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu.

. KUSULUHISHA MIGOGORO:

7.1 Wahusika wa Mkataba huu watatumia uwezo wao wenyewe kusuluhisha kwa amani migogoro na tofauti yoyote itakayojitokeza kati yao inayohusu utekelezaji wa Mkataba huu.

7.2 Endapo watashindwa kusuluhisha mgogoro au tofauti kati yao, mmoja wao atawasilisha mgogoro huo kwa msuluhishi kulingana na **Sheria ya Usuluhishi Na.2 ya mwaka 2020.**

7.3 Hatua ya mwisho itakuwa ni kwenda Mahakamani endapo wahusika watashindwa kusuluhisha mgogoro wao.

8. SHERIA ITAKAYOTUMIKA:

Mkataba huu utatafsiriwa na kuongozwa kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

9. MAELEKEZO/MAWASILIANO:

Maelekezo yanayotolewa na Mnunuzi yatakuwa kwa maandishi. Kwa sababu nyingine yoyote ile maelekezo hayo yanaweza yakatolewa kwa njia ya mdomo, Mzabuni atafuata maelekezo hayo. Katika muda usiozidi saa 72. Mnunuzi atatakiwa kuthibitisha kwa maandishi maelekezo aliyoyatoa awali kwa njia ya mdomo.

10. KUHAMISHA MKATABA/KUTOA KAZI KWA MZABUNI MSAIDIZI:

**Uhawilishaji:** Muuzaji hatahamisha jukumu lake la kimkataba iwe lote au sehemu ya majukumu yake kwa muuzaji mwingine kabla ya kupata idhini ya maandishi ya Mnunuzi.

11. VIFAA TIBA VINAVYOWEZA KUKATALIWA:

Vifaa tiba (blood gas analyzer) visivyo kidhi mahitaji, viwango na maelekezo ya Mnunuzi kama ilivyo elekezwa kwenye Mkataba vitakataliwa na Mnunuzi. Kwa maelekezo ya Mnunuzi, Mzabuni kwa gharama zake mwenyewe atabadilisha vifaa vya umeme vitakavyokuwa vimekataliwa hadi kumridhisha Mnunuzi kikamilifu. Endapo Mzabuni atashindwa kufanya marekebisho au mabadiliko ya vifaa vya Mfumo Wa Zimamoto vilivyo kataliwa kwa wakati, Mnunuzi atahesabu hasara itakayosababishwa na uzembe huo na mzabuni atawajibika kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 4.1 hapo juu.

**MABADILIKO YA BEI:**

Hakuna mabadiliko yoyote ya bei yatakayofanyika katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba huu.

13. **KUVUNJA MKATABA:**

13.1 Kama **Mzabuni** atashindwa kuanza kufanyakazi/ kutoa huduma katika muda uliopangwa au kuna sababu za kutosha kuamini kuwa hatakamilisha kutoa huduma yote katika muda uliopangwa au kuna ucheleweshaji uliokiuka tarehe na muda wa kukamilisha kutoa huduma au anashindwa kufuata moja ya masharti au hafuata maelekezo ya Mnunuzi au anakuwa mufilisi, Mnunuzi atakuwa na haki ya kuvunja mkataba na kutafuta **Mzabuni** mpya wa kufanya kazi hiyo.

14. **MALIPO BAADA YA MKATABA KUVUNJIKA:**

Kama Mkataba umevunjika, **Mzabuni** atalipwa na Mnunuzi fedha au maamuzi yatakayo kuwabado hayajalipiwa katika malipo atakayokuwa amelipwa **Mzabuni** kwa uletaji wa vifaa hivyo vyote vitakayokuwa vimetolewa kwa Mnunuzi kabla ya kuvunjika Mkataba kwa kima na bei kama ilivyotolewa kwenye Mkataba.

15. **TAMKO LA MZABUNI**

15.1. Mimi ......MONICA JOSEPH...... Ambaye ni ......CEO...... natamka wazi kwamba nimefanya utafiti wa kutosha kwa ajili ya Kufanya kazi/kutoa huduma hii ya uuzaji wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara kwa gharama ya **Tsh 19,500,000/= (Milioni Kumi na Tisa na Laki Tano Tu)**

15.2 Gharama zote hizo zinajumuisha uuzaji wa Vifaa tiba, Usafirishaji wa Vifaa, Kodi, kuvifunga na kufundisha watumiaji wa vifaa tiba hivyo na kwamba nisipotekeleza masharti ya mkataba huu ipasavyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yangu kwa mujibu wa mkataba huu. Pia natamka wazi kwamba MZABUNI sio mtumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara, na kwamba endapo itathibitika nimedanganya hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

**ILI KUTHIBITISHA MAKUBALIANO HAYA,** Wahusika wamesaini Mkataba huu kwa siku na tarehe kama inavyoonekana hapa chini:-

**KWA UPANDE WA MNUNUZI MKATABA HUU UMESAINIWA NA:**

JINA: KATHERINE MAGALI

CHEO: MGANGA MFAWIDHI

SAHIHI: [signature]

ANUANI: S.L.P. 577, BABATI

TAREHE: 08/04/2022

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA ... MANYARA
P.O BOX 577
BABATI-MANYARA

SHAHIDI:

JINA: AISHA ELIAS

CHEO: KATIBU WA AFYA

SAHIHI: [signature]

ANUANI: S.L.P 577, BABATI

TAREHE: 08/04/2022

**KWA UPANDE WA MZABUNI MKATABA HUU UMESAINIWA NA:**

JINA: MONICA JOSEPH

CHEO: CHIEF EXECUTIVE OFFICER

SAHIHI: [signature]

ANUANI: 1778, DAR-ES-SALAAM.

TAREHE: 08/04/2022

SHAHIDI:

JINA: ANNA RINGO

CHEO: ADMINISTRATIVE ASSISTANT

SAHIHI: [signature]

ANUANI: 1778, DAR-ES-SALAAM.

TAREHE: 08/04/2022

**MOKASI MEDICAL SYSTEMS & ELECTRONICS SERVICES LIMITED**

45/46 Chimara Street, Palm Residency Building GF
P.O. Box 1778 DAR-ES-SALAAM TANZANIA
Tel: +255 22 2924103 Fax: +255 22 2924106 Email: *info@mokasi.co.tz*
VAT 10-001065-X TIN 100-113-104

Proforma Invoice **No. 220404**

# PROFORMA INVOICE

Name: MANYARA REGIONAL REFERRAL HOSPITAL
Address: P. O. BOX 577
City: BABATI-MANYARA TANZANIA

Date 06th APR 2022
Order No.

| Qty | Type Number and Description | Unit Price | TOTAL (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | BLOOD GAS AND ELECTROLYTE ANALYZER i15 | | 18,510,000.00 |
| 1 | Test Cartridge BG10 (25Pcs/Pack) Blood Gas & Electro | | 660,000.00 |
| 1 | Calibrant Fluid Pack Cp 100 (100Test/Pack (11/22) | | 330,000.00 |

PROFORMA INVOICE

*Amount in words:* TZS. Nineteen Million Five Hundred Thousand Only.

SubTotal TZS 19,500,000.00

TOTAL TZS **19,500,000.00**

Validity: 30 days

Payment Terms: Pre- Payment

Bankers: Standard Chartered Bank Tanzania Limited
IHP Branch
Account No: 0102020534300
Dar-es-Salaam, TANZANIA

Mokasi Medical Systems & Electronics Services Ltd.

# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA

## MKATABA WA UNUNUZI WA VIFAA TIBA (BED SIDE CABINETS, CARDIAC TABLES, THREE FUNCTIONAL MANUAL HOSPITAL BEDS, BLOOD GAS ANALYZER) HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA

**BAINA YA**

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MANYARA**

**NA**

**ANUDHA LIMITED**

..................................................

Mkataba Huu Umeingiwa leo Tarehe ...08... Mwezi ...04...2022

KATI YA

**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara** (ambaye atajulikana kama Mnunuzi kwa upande mmoja.)

NA

**ANUDHA LIMITED** wa **S.L.P ......... Dar Es Salaam** (ambaye atajulikana kama Mzabuni kwa upande mwingine).

**KWA KUWA** Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara iko tayari na inania na Inahitaji Vifaa tiba Na kampuni ya ANUDHA LIMITED itahitajika uuzaji wa Vifaa hivyo vyote kwa masharti yatakayo ainishwa kwenye mkataba huu.

**NA KWA KUWA** kampuni iko tayari na inania na uwezo wa kuuza vifaa tiba hivyo kwa kuzingatia makubaliano na masharti kama yalivyoainishwa hapa chini.

**SASA WAHUSIKA WANAKUBALIANA YAFUATAYO;**

**1.0. MAELEZO YA VIFAA HIVYO**

1.1. Mkataba huu utakuwa ni usambazaji wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara.

1.2. Vifaa tiba ambavyo mzabuni ataleta katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara ni kama ilivyo orodheshwa hapa chini:-

| **Na** | **Aina ya kifaa** | **Idadi** | **Gharama/moja** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Bed side cabinets | 22 | 250,000 | 5,500,000.00 |
| 2 | Cardiac tables | 19 | 300,000 | 5,700,000.00 |
| 3 | Three functional manual hospital beds | 19 | 1,800,000 | 34,200,000.00 |
| 4 | Blood gas analyzer | 1 | 19,000,000 | 19,000,000.00 |
| | ufungaji na mafunzo | | | 1,000,000.00 |
| | Usafirishaji, | | | 2,900,000.00 |
| | **Jumla** | | | **68,300,000.00** |

**NA KWA KUWA** Mzabuni yuko tayari na ana uwezo wa kufanya kazi hiyo:

**HIVYO BASI, WAHUSIKA WANAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

**1: MAELEZO YA KAZI.**

Kazi zinazotakiwa kufanyika ni kama ifuatavyo:

a) Kusambaza vifaa tiba (bed side cabinets, cardiac tables, three functional manual hospital beds, blood gas analyzer) mpaka eneo husika.

b) Kuvifunga na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa vifaa tiba husika

c) Vifaa tiba vitakavyouzwa viwe vimekidhi viwango vya ubora kama ulivyoelekezwa kwenye nukuu za bei.

**2: MUDA WA KUKAMILISHA KAZI/MUDA WA MKATABA.**

**Mzabuni** amekubaliana na **Mnunuzi** kuleta vifaa tiba tajwa hapo juu ndani ya miezi miwili, kuanzia pale mkataba utakapo sainiwa. Ieleweke wazi kuwa **Mzabuni** akishindwa kukamilisha kazi/usambazaji wa vifaa vya Umeme kwa muda waliokubaliana na **Mnunuzi**, atawajibika kumlipa Mnunuzi fidia ya ucheleweshaji (liquidated damage) ya asilimia moja (1%) ya gharama kwa siku kwa kila siku inayoongezeka baada ya kuvunja kipengele hiki cha Mkataba hadi atakapokamilisha kazi husika.

**3. MALIPO KWA MZABUNI:**

Mzabuni atalipwa malipo yake yote pale tu atakapomaliza kuleta vifaa vyote katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara na Hospitali kukagua na kujiridhisha kuwa vifaa vilivyoletwa vipo kwa mujibu wa mkataba wake ndipo Mzabuni atalipwa malipo yake ambayo ni kiasi cha **Tsh 68,300,000/=(Milioni Sitini na nane na laki tatu tu).**

Mzabuni atalipwa malipo ya awali (ADVANCE PAYMENT) ambayo ni asilimia 30 ya gharama yote.

**MAJUKUMU YA WAHUSIKA:**

**4.1 Majukumu ya Mzabuni**

**Mzabuni atatakiwa:**

(a) Kutoa Huduma inayohitajika na Mnunuzi kwa wakati na muda waliokubaliana.

(b) Kutoa Huduma kwa viwango vilivyooneshwa na ubora unaotakiwa na Mnunuzi

(c) Kuzingatia suala la muda katika kutekeleza huduma hiyo.

(d) Kuzingatia uangalifu, uadilifu na uaminifu wakati wa kutekeleza Mkataba huu. Itakapobainika kuna udanganyifu katika kutekeleza kazi hii kinyume na makubaliano yaliyomo kwenye Mkataba huu, Mzabuni atalazimika kurejesha gharama zote za Mkataba huu na kufikishwa katika vyombo vya Sheria kwa hatua za kisheria zaidi;

**4.2 MAJUKUMU YA MNUNUZI.**

**Mnunuzi atatakiwa:**

(a) Kumuwezesha Mzabuni kuwa na mazingira mazuri katika utekelezaji wa Mkataba huu, ikiwa ni pamoja na kukagua ubora wa huduma na kutoa ushauri au maelekezo pale inapohitajika kulingana na mahitaji ya Mnunuzi.

(b) Kumlipa Mzabuni stahiki yake kama makubaliano yalivyo. Ieleweke kuwa Mnunuzi hatalipa malipo yoyote Kwa Mzabuni kabla ya kukamilisha kuleta vifaa kulingana na Mkataba huu. Aidha, Mnunuzi hatalipa kiasi chochote cha malipo kwa Mzabuni kama Mzabuni atashindwa kukamilisha kazi kwa wakati kulingana na Mkataba badala yake Mzabuni atatakiwa kulipa fidia ya ucheleweshaji vifaa kwa Mnunuzi.

(c) Kukagua Vifaa tiba vinavyoletwa na Mzabuni na kutoa ushirikiano unaofaa wakati Mnunuzi atakapohitaji kufanya hivyo.

**5. MATUKIO YASIYOTARAJIWA (FORCE MAJEURE)**

5.1 Matukio yasiyotarajiwa ***(FORCE MAJEURE)*** yana maana ya matukio yaliyo nje ya uwezo wa wahusika na ambayo hawakuweza kuyaona wakati wa kusaini Mkataba huu, ambapo matokeo yake yatasababisha Mzabuni asiweze kutekeleza Mkataba huu. Matukio hayo ni kama vita, vita vya kikabila, moto, mafuriko, mgomo, magonjwa ya mlipuko, Mabadiliko ya Sheria na mengineyo.

5.2 Matukio haya yatakapotokea wahusika wa Mkataba huu wataahirisha utekelezaji wa Mkataba huu bila kuwajibika kwa hasara itakayotokana na tukio husika, kwa kipindi na eneo linalohusika na lililoathiriwa na tukio husika.

5.3 Wahusika wa Mkataba huu watapeana taarifa haraka iwezekenavyo kabla ya kusimamisha kazi/ huduma. Kama taarifa ya awali imetolewa kwa njia isiyo ya maandishi, ndani ya masaa 24 taarifa iliyotolewa kwa njia isiyo ya maandishi itolewe kwa maandishi. Mawasiliano yote ya maandishi yatawasilishwa kwenye ofisi ya Mnunuzi na siyo sehemu nyingine yoyote.

## 6. UWAJIBIKAJI WA WAHUSIKA.

6.1 Mzabuni atawajibika kwa hasara, uharibifu na gharama zinazotokana na uzembe wake mwenyewe, mawakala wake au wafanyakazi wake wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu.

6.2 Mnunuzi hatawajibika kwa hasara au uharibifu wowote utakaotokana na uzembe wa Mzabuni mwenyewe au Mawakala wake au wafanyakazi wake wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu.

## 7. KUSULUHISHA MIGOGORO:

7.1 Wahusika wa Mkataba huu watatumia uwezo wao wenyewe kusuluhisha kwa amani migogoro na tofauti yoyote itakayojitokeza kati yao inayohusu utekelezaji wa Mkataba huu.

7.2 Endapo watashindwa kusuluhisha mgogoro au tofauti kati yao, mmoja wao atawasilisha mgogoro huo kwa msuluhishi kulingana na **Sheria ya Usuluhishi Na.2 ya mwaka 2020.**

7.3 Hatua ya mwisho itakuwa ni kwenda Mahakamani endapo wahusika watashindwa kusuluhisha mgogoro wao.

**SHERIA ITAKAYOTUMIKA:**

Mkataba huu utatafsiriwa na kuongozwa kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**9. MAELEKEZO/MAWASILIANO:**

Maelekezo yanayotolewa na Mnunuzi yatakuwa kwa maandishi. Kwa sababu nyingine yoyote ile maelekezo hayo yanaweza yakatolewa kwa njia ya mdomo, Mzabuni atafuata maelekezo hayo. Katika muda usiozidi saa 72. Mnunuzi atatakiwa kuthibitisha kwa maandishi maelekezo aliyoyatoa awali kwa njia ya mdomo.

**10. KUHAMISHA MKATABA/KUTOA KAZI KWA MZABUNI MSAIDIZI:**

**Uhawilishaji:** Muuzaji hatahamisha jukumu lake la kimkataba iwe lote au sehemu ya majukumu yake kwa muuzaji mwingine kabla ya kupata idhini ya maandishi ya Mnunuzi.

**11. VIFAA TIBA VINAVYOWEZA KUKATALIWA:**

Vifaa tiba (bed side cabinets, cardiac tables, three functional manual hospital beds, blood gas analyzer) visivyo kidhi mahitaji, viwango na maelekezo ya Mnunuzi kama ilivyo elekezwa kwenye Mkataba vitakataliwa na Mnunuzi. Kwa maelekezo ya Mnunuzi, Mzabuni kwa gharama zake mwenyewe atabadilisha vifaa vya umeme vitakavyokuwa vimekataliwa hadi kumridhisha Mnunuzi kikamilifu. Endapo Mzabuni atashindwa kufanya marekebisho au mabadiliko ya vifaa vya Mfumo Wa Zimamoto vilivyo kataliwa kwa wakati, Mnunuzi atahesabu hasara itakayosababishwa na uzembe huo na mzabuni atawajibika kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 4.1 hapo juu.

**12. MABADILIKO YA BEI:**

Hakuna mabadiliko yoyote ya bei yatakayofanyika katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba huu.

**13. KUVUNJA MKATABA:**

13.1 Kama **Mzabuni** atashindwa kuanza kufanyakazi/ kutoa huduma katika muda uliopangwa au kuna sababu za kutosha kuamini kuwa hatakamilisha kutoa huduma yote katika muda uliopangwa au kuna ucheleweshaji uliokiuka tarehe na muda wa kukamilisha kutoa huduma au anashindwa kufuata moja ya masharti au hafuata maelekezo ya Mnunuzi au anakuwa mufilisi, Mnunuzi atakuwa na haki ya kuvunja mkataba na kutafuta **Mzabuni** mpya wa kufanya kazi hiyo.

**14. MALIPO BAADA YA MKATABA KUVUNJIKA:**

Kama Mkataba umevunjika, **Mzabuni** atalipwa na Mnunuzi fedha au maamuzi yatakayo kuwabado hayajalipiwa katika malipo atakayokuwa amelipwa **Mzabuni** kwa uletaji wa vifaa hivyo vyote vitakavyokuwa vimetolewa kwa Mnunuzi kabla ya kuvunjika Mkataba kwa kima na bei kama ilivyotolewa kwenye Mkataba.

**15. TAMKO LA MZABUNI**

15.1. Mimi ......ANURAG HASSIJA...... Ambaye ni ......MKURUGENZI natamka wazi kwamba nimefanya utafiti wa kutosha kwa ajili ya Kufanya kazi/kutoa huduma hii ya uuzaji wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara kwa gharama ya **Tsh 68,300,000/=(Milioni Sitini na nane na laki tatu tu)**

15.2 Gharama zote hizo zinajumuisha uuzaji wa Vifaa tiba, Usafirishaji wa Vifaa, Kodi, kuvifunga na kufundisha watumiaji wa vifaa tiba hivyo na kwamba nisipotekeleza masharti ya mkataba huu ipasavyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yangu kwa mujibu wa mkataba huu. Pia natamka wazi kwamba MZABUNI sio mtumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara, na kwamba endapo itathibitika nimedanganya hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

**ILI KUTHIBITISHA MAKUBALIANO HAYA,** Wahusika wamesaini Mkataba huu kwa siku na tarehe kama inavyoonekana hapa chini:-

**KWA UPANDE WA MNUNUZI MKATABA HUU UMESAINIWA NA:**

**JINA:** KATHERINE MAGALI

**CHEO:** MGANGA MFAWIDHI

**SAHIHI:** ...........................

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA
P.O.BOX 577
BABATI-MANYARA

**ANUANI:** S.L.P. 577, BABATI

**TAREHE:** 08/04/2022

**SHAHIDI:**
**JINA:** AISHA ELIAS

**CHEO:** KATIBU WA AFYA

**SAHIHI:** ...........................

**ANUANI:** S.L.P 577, BABATI

**TAREHE:** 08/04/2022

**KWA UPANDE WA MZABUNI MKATABA HUU UMESAINIWA NA:**

**JINA** ANDREA HASSAN

**SAHIHI:** ...........................

ANUDHA LIMITED
P.O.Box 5982
DAR-ES-SALAAM
TEL: 2122745, 2122747
FAX: 2126490

**ANWANI:** S.L.P 5982 DSM

**TAREHE:** 02-04-2022

**SHAHIDI:**
**JINA:** CYPRIAN MWAGIKE

**SAHIHI:** ...........................

**CHEO:** AFISA MASOKO

**ANWAN:** S.L.P 5982 DSM

**TAREHE:** 02-04-2022